a YOUTH:WORK program

## CHANGAMOTO

Kutokana na madhara ya kijamii yatokanayo na janga la ugonjwa wa UKIMWI, mamilioni ya watoto walioathirika na VVU wanaishi katika mazingira magumu na kuna uwezekano wa kuwa wahanga wa unyanyasaji kama kuishi katika taasisi za kutoa huduma au mitaani na kushiriki katika ajira hatarishi na zenye madhara. Vijana wanaoishi na VVU/UKIMWI au walioathirika na VVU/UKIMWI wanakumbwa na changamoto nyingine maalum wanapojaribu kujenga maisha yao ya baadaye. Takribani asilimia 10% ya vijana wa Kitanzania wenye umri chini ya miaka 18 ni yatima na/au wanaishi katika mazingira magumu na wanakosa fursa ya kupata elimu muhimu na mafunzo kwa vitendo katika mpito wa kuelekea katika mafanikio ya baadaye. Mara nyingi vijana hawa wanakosa fursa za kusoma kutokana na kukosa fedha za kufidia gharama za shule au kuzidiwa na majukumu ya shughuli za nyumbani au shughuli zenye kuingiza kipato. Kitendo cha kumaliza elimu ya sekondari au elimu ya mafunzo kwa vitendo kitasaidia vijana wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na familia zao kujipatia njia ya kuondokana na umaskini.

## MALENGO MAHSUSI/HATUA ZILIZOZINGATIWA

Katika kukabiliana na changamoto hizi shirika la "International Youth Foundation" (IYF) linatekeleza mradi unaotambulika kama "Tanzania Youth Scholars", hatua ya kutoa fursa kwa watoto/vijana yatima na wale wanaoishi katika mazingira magumu (OVC) wenye umri kati ya miaka 14 hadi 24 kwa kuwapa udhamini wa kusoma sekondari au kusoma mafunzo ya ufundi na kuandaa hatima yao ya baadaye katika kujipatia ajira binafsi au kuajiriwa. Kwa ufadhili wa Shirika la Kimataifa la Maendeleo la watu wa Marekani (USAID) pamoja na mpango wa dharura wa Raisi wa Marekani wa kupunguza UKIMWI (PEPFAR) kupitia ubalozi wa Tanzania, TYS ilitunikiwa tuzo kupitia IYF's "Youth:Work Leader award" (tuzo kwa shirika linalofanya kazi na vijana) kwa makubaliano ya washirika wa Kimataifa na USAID. Mpango huu wa miaka mitano, ulizinduliwa mwezi Mei 2011; pia unajenga uwezo kwa mashirika ya Kitanzania kusimamia miradi ya ufadhili; na kutoa mafunzo na kufuatilia vijana wanaoishi katika mazingira magumu kwa ufanisi zaidi.

Kwa kupitia ushirikiano uliojengeka na mashirika ya ndani ya Tanzania ikiwemo "Campaign for Female Education" (Camfed) na "Vocational Training Authority" (VETA), mradi wa TYS unakuza na kutekeleza dhana yenye kiwango kikuu, inaonyesha matokeo na yenye hatua endelevu za kujikimu kimaisha ambazo zinajenga mbinu bora za kushughulikia mahitaji ya yatima na vijana walio katika mazingira magumu Tanzania. Kama sehemu ya hatua zilizochukuliwa, washiriki wa TYS wanawezeshwa kwa kupewa elimu ya afya ya uzazi na stadi za maisha ambazo ni muhimu kwa ajili ya kuboresha afya zao wenyewe na ustawi pamoja na kutoa michango chanya katika nguvu kazi, familia na jamii.

## MIKAKATI

Mradi huu umejumuisha vipengele vitatu:

- **Kufanikisha shughuli mbalimbali za vijana**; TYS imeundwa kutoa mafunzo ya kina na huduma za kuboresha uwezo wa kiafya na uzalishaji kwa yatima na waishio katika mazingira magumu. Pamoja na misingi iliyopo ya utatuzi kwa njia ya kutoa mafunzo ya ufundi na elimu ya sekondari na washiriki watapata mafunzo ya stadi za maisha, afya ya uzazi na elimu ya ujasiriamali ikiwemo msaada wa kisaikolojia na kuwandaa na ajira kupitia mafunzo kwa vitendo.
- **Kujenga Uwezo**; TYS inafanya kazi ya kujenga uwezo wa mashirika ya Kitanzania kuweza kukidhi mahitaji ya elimu na ajira kwa vijana wa Kitanzania wanaoishi katika mazingira magumu ili kukabiliana na mahitaji ya soko la ajira, shughuli za kujenga uwezo ni pamoja na kuendesha mafunzo kwa wakufunzi katika sehemu ya stadi za maisha, afya ya uzazi na ujasiriamali; kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini na shughuli za usimamizi wa fedha katika mashirika na kukuza uwezo wa mashirika kutoa huduma sahihi kwa yatima na walio katika mazingira magumu.
- **Kukuza ushirikiano wenye tija**; Kama sehemu ya mkakati wa utekelezaji wa TYS, IYF na wadau wake watashirikiana kwa karibu na mamlaka ya serikali za mitaa, viongozi wa kijamii, walimu, washauri na wazazi/walezi pamoja na mashirika yanayofadhiliwa na mfuko wa USAID katika kukuza wigo wa huduma zitolewazo kwa yatima na walio katika mazingira

*(continued)*

magumu na kujenga umiliki wa mradi huu kwa jamii. IYF inatazamia kuunda ushirikiano katika sekta ya umma na binafsi ili kuziba pengo katika utoaji huduma na kukuza rasilimali zinazotokana na matokeo ya mradi.

## MATOKEO TARAJIWA

Matokeo yafuatayo yanatarajiwa kupatikana kufikia mwisho wa mradi:

- Kufikia idadi ya yatima na vijana walio katika mazingira magumu 1,800 wenye umri kati ya 14 hadi 24 waliopata fursa ya elimu bora ya ufundi na elimu ya sekondari kupitia ufadhili na misaada mingine iliyotolewa.
- Wadau kuboreshewa uwezo wao wa kutoa mafunzo yenye kiwango cha juu kulingana na soko la ajira na msaada wa kielimu kwa yatima na vijana walio katika mazingira magumu.
- Kuongezeka kwa fursa za ajira kwa vijana waliohitimu na kupata mitaji na misaada mingine kwa wajasiriamali wadogo kutokana na ubia au ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi.
- Jamii na uongozi wa serikali za mitaa kutambua na kuwasaidia yatima na vijana walio katika mazingira magumu kufanikisha vizuri fursa ya elimu au mafunzo ya ufundi waliyoyapata.

## USHIRIKISHWAJI

Kuchangia kwa njia isiyo ya kifedha au ya kutoa rasilimali fedha (kwa hali na/au mali)? Kutokana na kujenga ubia katika sekta za umma na binafsi ni jambo la muhimu katika juhudi zetu za kuboresha maisha na matarajio ya watoto Watanzania haswa yatima na waishio katika mazingira magumu. Tunawakaribisha mtuunge mkono katika kufikia mahitaji ya vijana kwa kuchangia katika kufanikisha mradi wa TYS.

Jinsi ya Kuchangia ...

- Kutoa nafasi za ajira kwa washiriki wa TYS katika mafunzo kwa vitendo au kuwaajiri.
- Kuchangia vifaa vinavyohitajika kwa mafunzo ya ufundi au vifaa vingine vitavyomwezesha kijana akuze ujuzi wake.
- Kutoa huduma nafuu ya afya kama ushauri nasaha na kupima.
- Kuchangia vifaa vya shule au vya usafi kwa washiriki wa bweni wa TYS katika vituo vya mafunzo.
- Kujenga uwezo kwa wadau wanaotekeleza mradi wa TYS kwa njia ya warsha mbalimbali katika huduma ya saikolojia, ulinzi wa watoto au tathmini na ufuatiliaji na zinginezo.
- Kwa kushirikisha uzoefu na utaalamu wako kwa kuwa mzungumzaji katika shule au vituo vya mafunzo ya ufundi vinavyofadhiliwa na TYS.
- Kwa kutoa mtaji wa kuanzisha biashara au kwa kuwa mshauri kwa wajasiriamali wadogo.

Timu ya TYS watafurahi kuzungumzia njia hizi mbadala au njia yeyote ambayo wewe au shirika lako litakavyoweza kuchangia katika kuboresha matarajio ya vijana wa Kitanzania wanaoishi katika mazingira magumu.

## KWA MAWASILIANO

*Sarah Shebele, Program Director, Dar es Salaam*
Email: s.shebele@iyfnet.org

*Matthew Breman, Director, Africa Programs, Baltimore*
Email: m.breman@iyfnet.org

PARTNERS

LOCAL PARTNERS